Hatua za busara ya COVID kwa shule

Habari kwa familia

Tunajua kwamba kuwepo pamoja darasani ni jambo bora kwa kujifunza, ukuaji na ustawi wa wanafunzi wetu. Muhula huu tutaendelea kutekeleza hatua kadhaa ili kutuwezesha kuweka kipaumbele ustawi wa wanafunzi wetu pamoja na mazingira thabiti na yenye tija ya kujifunza.

Kaa nyumbani ikiwa unajisikia kuumwa

- Ikiwa mtoto wako anajisikia kuumwa, lazima umweke nyumbani. Ikiwa anaonyesha hata dalili ndogo za COVID-19, anapaswa kupimwa kwa kipimo cha COVID na kujitenga.
- Mtoto wako anapaswa kurudi shuleni tu mara anapopokea matokeo hasi na hana dalili zozote.
- Ikiwa mtoto wako anapimwa chanya kwa COVID-19, andikisha matokeo chanya na Huduma ya NSW (Service NSW), ajitenge kwa siku 7 na ufuate miongozo ya afya ya NSW.

Chanjo

- Chanjo ya COVID-19 na homa ya mafua ni njia bora ya kujilinda, familia yako na jumuiya yako. Chanjo ni njia ya salama na yenye ufanisi ili kukupa mfumo wako wa kinga msaada dhidi ya magonjwa ya virusi.
- Wafanyakazi wote wanaostahiki katika mipangilio ya shule za kawaida na wanafunzi wanahimizwa sana kusasisha na chanjo zao ili kulinda afya zao. Wafanyakazi wote wanaofanya kazi shuleni kwa madhumuni maalum wanatakiwa kuchanjwa mara mbili dhidi ya COVID-19 kuwalinda wanafunzi wetu ambao wako katika hatari kubwa ya ugonjwa mbaya ikiwa wanahatarishwa kwa COVID-19.

Mawasiliano wa karibu na mgonjwa

- Wanafunzi waliotambuliwa kama watu wanaowasiliana nao wanaweza kuhudhuria shule ikiwa shule itaarifiwa na wakionyesha matokeo hasi ya kipimo kuwa hawana COVID-19 kila asubuhi kabla ya kuhudhuria shule kwa siku 5 za shule.
- Wanafunzi wa shule ya sekondari wanapaswa kuvaa maski katika maeneo ya ndani isipokuwa wakati wanapokula au kufanya mazoezi. Wanafunzi wa shule ya msingi wanapendekezwa kuvaa maski ndani ya nyumba isipokuwa wakati wanapokula au kufanya mazoezi.
- Wanafunzi waliotambuliwa kuwa mawasiliano wa karibu hawataruhusiwa kabisa kuhudhuria mazingira yenye hatari kubwa kama vile safari za usiku au kambi za shule.
- Wanafunzi katika shule za madhumuni maalum na vitengo vya usaidizi hawawezi kuhudhuria shule kama waliokuwa karibu na mgonjwa na watasaidiwa kujifunza kwa mbali wakati wa kujitenga.

Upimaji wa haraka wa antijeni

- Vipimo vya haraka vya antijeni vinapaswa kutumiwa ikiwa mtoto wako anaonyesha hata dalili ndogo za COVID-19, au kila siku ikiwa wanahudhuria shule kama mtu wa karibu.
- Ikiwa mtoto wako anapimwa chanya kwa COVID-19, lazima asihudhurie shuleni mpaka kipindi chake cha kujitenga kinamaliza na hana dalili zozote. Matokeo chanya ya kipimo cha haraka cha antijeni lazima yaandikishwe na Huduma ya NSW (Service NSW).
- Ikiwa mtoto wako anapimwa hasi lakini bado anaonyesha dalili anapaswa kutohudhuria shuleni hadi hana dalili zozote.
- Wafanyakazi na wanafunzi watapewa paketi 1 ya vifaa 5 vya kupima antijeni haraka na shule yao katika Kipindi cha 3 mapema. Wafanyakazi na wanafunzi wa shule za madhumuni maalum na vitengo vya usaidizi watapewa paketi 2 za vifaa 5 vya kupima antijeni haraka na shule yao katika Kipindi cha 3 mapema.
- Shule zitadumisha hifadhi ya akiba ya vipimo vya haraka ya antijeni katika maeneo ya shule kwa madhumuni ya uchunguzi wa upimaji iwapo ikitokea mlipuko.

Usafi na kusafisha

- Wanafunzi wanahimizwa kunawa mikono kila mara kwa sabuni na maji na kutumia vifaa vya kinga binafsi inapotakiwa.
- Usafishaji ulioimarishwa wa siku wa shule utazingatia maeneo ya mguso wa juu na nyuso ngumu zingine, vishiko vya mlango, makabati, swichi za mwanga na vishiko vya ngazi katika ngazi na maeneo ya harakati.

Uingizaji hewa

- Hewa safi ni njia bora zaidi ya uingizaji hewa kupunguza hatari ya maambukizo.
- Katika miezi ya baridi, inapokanzwa itatumika kushirikiana na njia za uingizaji hewa kusawazisha faraja ya joto.
- Nafasi zote za kujifunza katika shule za serikali zimeangaliwa kuhakikisha viwango vinavyofaa vya uingizaji hewa na vifaa vya kusafisha hewa vimetolewa pale inapohitajika.
- Kutumia nafasi za nje kutaendelea kuhimizwa inapowezekana.

Maski

- Kuvaa maski kunahimizwa sana inapowezekana kwa wafanyakazi na wanafunzi wote katika maeneo ya shule za kawaida, hasa katika nafasi za ndani na matukio mengine ambapo uingizaji hewa na kukaa mbali hauwezekani.
- Maski zinatakiwa kwa wafanyakazi wote wanaofanya kazi na wanafunzi katika hatari kubwa ya ugonjwa mbaya ikiwa wataambukizwa COVID-19.
- Kuvaa maski kunahimizwa sana kwa wageni, haswa wanapowasiliana moja kwa moja na wanafunzi, na kunatakiwa wanapowasiliana na wanafunzi ambao wako hatari kubwa wa ugonjwa mbaya wakiambukizwa COVID-19.
- Maski zinahitajika ikiwa ndani ya nyumba kwa wanafunzi wanaohudhuria shule kama watu wa karibu katika Mwaka wa 7 na zaidi na wanahimizwa sana kwa wanafunzi wadogo.
- Uvaaji wa maski unahimizwa sana kwa wanafunzi wote kwa siku 3 baada ya kupona kwao COVID-19.

Wageni

- Wageni wanaweza kuhudhuria maeneo ya shule za kawaida bila kujali hali yao ya chanjo.
- Wageni wote wanahimizwa sana kuvaa maski, haswa ndani ya nyumba au wakati kukaa mbali hakuwezekani, na wakati wa kuingiliana moja kwa moja na wanafunzi.
- Wageni kwa shule kwa madhumuni maalum na vitengo vya usaidizi, wakiwemo wafanyakazi na watu wanaojitolea, lazima wavae maski ikiwa wanawasiliana moja kwa moja na wanafunzi.
- Wageni wanaohudhuria shule kama waliokuwa karibu na mgonjwa wa korona wanatakiwa kuifahamisha shule na kufuata miongozo fulani, ikiwemo kuvaa maski wakati wako ndani nyumba. Wageni waliokuwa karibu na mgonjwa hawawezi kuhudhuria shule za madhumuni maalum.

Shughuli

- Tathmini za hatari za afya na usalama zitaunganishwa katika shughuli za kupanga, ikijumuisha safari na kambi za usiku.
- Wazazi na walezi watafahamishwa kuhusu hatari ya kuambukizwa na watahitaji kutoa ruhusa kwa shughuli fulani.

Kujibu hali za ndani

- Shule zitafanya kazi na timu ya idara ya usimamizi wa kesi ya Afya, Usalama na Ustawi wa Wafanyakazi ili kujibu ipasavyo hali za ndani, ikiwa ni pamoja na milipuko ya magonjwa ya virusi.
- Katika baadhi ya kesi, shule zinaweza kuanzisha hatua za ziada kwa muda mfupi ili kusaidia kukomesha kueneza kwa maambukizi, zikijumuisha kutakiwa kuvaa maski, kuchelewesha au kuahirisha au kupunguza shughuli zisizo muhimu na kuelekeza vikundi fulani kujifunza kwa mbali.

Kujifunza kwa mbali

- Idara inaendelea kutengeneza nyenzo za kidijitali za kujifunzia ili kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji kujifunza wakiwa mbali.

Kwa habari zaidi, tembelea education.nsw.gov.au/covid-19/advice-for-families

Huduma ya Mkalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji maelezo zaidi tafadhali pigia simu mkuu wa shule yako. Kama ukihitaji mkalimani kukusaidia na swali lako tafadhali piga simu Huduma ya Mkalimani wa Simu kwenye 131 450 na omba kwa mkalimani katika lugha yako. Mwambie opereta nambari ya simu unayotaka kupiga simu, na opereta atapata mkalimani kwenye laini ili kukusaidia kwa mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.

Serikali ya NSW inaahidi kuhakikisha shughuli za shule zinaendelea huku ikiweka kipaumbele usalama na ustawi wa wanafunzi na wafanyakazi wa shule.